YOUTH ACTION VOLUNTEERS (YAV)

MAONI YETU JUU YA RIPOTI YA UKAGUZI WA FEDHA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII KWA MWAKA WA FEDHA 1998/99 – 2006/07

Utangulizi

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilianzishwa chini ya Ibara ya 143, ibara ndogo ya 5 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005 kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu za serikali na asasi nyingine za umma. Sheria ya Fedha namba 6 ya mwaka 2001 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004 inampa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu mamlaka ya kukagua hesabu za asasi za umma angalau mara moja kila mwaka.

Uchambuzi huu unapitia kwa kina ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi yamechukuliwa kama taarifa sahihi katika kupima uwajibikaji kifedha wizarani.

Toleo jipya la ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi inapendekeza uboreshaji wa jumla wa usimamizi wa fedha serikalini (soma Jedwali 1). Kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2006/2007, hati safi zimeongezeka kutoka asilimia 57 hadi asilimia 77, wakati hati chafu zimepungua kutoka asilimia 39 hadi 26 na hati zenye hitilafu zimepungua kutoka asilimia 4 hadi sifuri.

Jedwali 1: Mwelekeo wa hesabu za serikali, mwaka wa fedha 2005-07

	Hati Safi		Hati Chafu		Hati zenye hitilafu		Jumla
	05/06	06/07	05/06	06/07	05/06	06/07	05/07
MDA	24	37	22	12	3	-	49
RAS	16	15	6	6	-	-	21
Jumla	40	52	27	18	3	-	70
Asilimia	57	74	39	26	4		100

Chanzo: www.nao.go.tz
MDA= Wizara, Idara na Wakala
RAS= Katibu Tawala Mkoa

Mtazamo wa jumla wa jedwali hapo juu, unasomeka kwamba kuna maendeleo chanya katika kushughulikia hitilafu za kihesabu. Hata hivyo katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaonekana hakuna mabadiliko makubwa katika miaka miwili iliyopita (2005/06, 2006/07) katika kushughulikia hitilafu za kihesabu. Kutokana na uchambuzi uliofanywa kuhusu mapendekezo yaliyotolewa kwa Wizara, Idara na Wakala kwa mwaka wa fedha 2005/06 na 2006/07, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilipata hati chafu katika miaka yote miwili. Wizara, Idara na Wakala (12) (17%) zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2005/06 zilipatiwa hati chafu, wakati Wizara, Idara na Wakala 24 (45%) zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2006/07 zilipatiwa hati chafu. Aina hii ya hati hutolewa pale Mdhibiti na Mkaguzi anapokuta hali ya kutowiana maelezo ya utawala au hali zisizoeleweka zenye athari katika vitu lakini zisizo za msingi katika taarifa za fedha.
Ripoti mpya inaonyesha Wizara, Idara na Wakala/ Katibu Tawala Mkoa wamepiga hatua katika kushughulikia hitilafu za kihesabu za miaka iliyopita.

Uchambuzi huu ni wa hesabu za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 1999/2000 hadi 2006/07. Muhtasari wa hitilafu unapatikana **Jedwali 2.**

Jedwali 2: Muhtasari wa Hitilafu kutoka Hesabu Zilizokaguliwa za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii 1998/99 hadi 2006/07

Na	**Hitilafu**	**Mwaka wa fedha (Shilingi milioni)**								
		1998/99	**1999/00**	**2000/01**	**2001/02**	**2002/03**	**2003/04**	**2004/05**	**2005/06**	**2006/07**
1	Malipo yenye utatas	56.4	_	158.6	101.8	156.8	561.0	_	56.8	_
2	Matibabu nje ya nchi	1,300.0	673.1	732.1.	733.5	_	_	_	255.4	_
3	Mishahara isiyochukuliwa	6.9	_	_	_	_	_	_	_	_
4	Mishahara ambayo haikuombwa	5.0	_	20.8	5.4	_	_	_	_	_
5	Masurufu maalum	356.1	_	749.1	1,000.0	1,100.0	_	949.5	1,100.0	750.2
6	Ubora wa Ankara kifani	134.3	_	_	_		_	_	_	_
7	Vilivyopotea stoo	132.0	152.0	850.2	166.9	58.2	_	_	_	_
8	Matumizi yasiyo na vocha na yenye vocha zilizokosewa	22,200.0	17,400.0	3,094.4	3,600.0	5,700.0	16,600.0	30,000.0	7,829.7	565
9	Tofauti katika daftari la fedha	217.0	_	_	_	_	_	_	3,860.0	_

Chati 1 inaonyesha mwelekeo wa matumizi yasiyo na vocha na yenye vocha zilizokosewa.

Matumizi yasiyo na vocha na yenye vocha zilizokosewa yalipungua kwa kiasi kikubwa kati ya mwaka 1998/99 na 2000/01, yalirudi tena 2004/05, na lakini yamepungua tena katika miaka miwili ya mwisho ya fedha. Haya ni mafanikio kwa upande wa wizara. Malipo ambayo yalipingwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ni pamoja na Shilingi milioni 20 kwa ajili ya huduma ya ushauri ambao haukotolewa katika mwaka wa fedha 2004/05 na magari yenye thamani ya Shilingi milioni 242 ambayo hayakuwasilishwa. Katika mwaka wa fedha 2005/06 kulikuwa na matumizi yasiyo ya lazima ya Shilingi milioni 150 kwa ajili ya kuchapisha mwongozo wa malaria, bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 36 hazikuwasilishwa pia kulikuwa na suala ya ununuzi wa magari yenye thamani ya Shilingi milioni 57.

Katika jedwali la muhtasari wa hitilafu za kihesabu hapo juu inaonekana kwamba idadi ya hitilafu (jedwali 2) kwa mwaka 2006/07 imepungua ikilinganishwa na miaka iliyotangulia lakini Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeendelea kupata hati chafu. Hati hii inachangiwa na;

Uwezo mdogo wa kihasibu

- malipo yasiyo na vocha na yenye vocha zilizokosewa yanafikia kiasi cha Shilingi 565, 030,363
- Orodha ya mali zinazohamishika haiwiani na mali zisizohamishika zinazomilikiwa na wizara
- Maelezo kuhusu mali na dhima haikuwa imeandaliwa

Kutoelewana juu ya namna bora ya kuhifadhi taarifa na kutofuata taratibu na sheria
• Masurufu ya kazi maalumu yenye thamani ya Shilingi 750, 239,060 hayakuwekwa kwenye vitabu vya fedha.
• Kuna mapato yaliyokusanywa ya Shilingi Shs.1, 237,408,995
• Malimbizo ya mapato ambayo hayakuripotiwa Shilingi108, 516,140
• Bidhaa zilizolipiwa bila kuwasilishwa 8,103,130,448.

Bunge kama chombo cha usimamizi.

Ndani ya Bunge la Tanzania, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ina jukumu la kusimamia masuala kuhusiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Wajibu wa kamati hii ni pamoja na:

- Kupitia bajeti ya wizara
- Kupitia ripoti ya mwaka ya ukaguzi
- Kufuatilia hatua zinazochukuliwa na wizara.

Kamati ya Huduma za Jamii hufuatilia bajeti na matumizi ya wizara lakini haina nguvu kunapokuwa na upungufu katika usimamizi wa fedha, ubadhilifu, udanganyifu unaobainishwa na ripoti za ukaguzi za kila mwaka.

Hitimisho

Je mchakato mzima wa ukaguzi wa hesabu na usimamizi wa bunge vinaleta nidhamu ya fedha na uwajibikaji? Raisi Kikwete wa Tanzania amebainisha kwamba ripoti za ukaguzi zinapaswa kupewa umuhimu wa ziada. Matokeo tuliyoona ni kwamba ripoti za ukaguzi hazitazamwi inavyostahili. Watendaji wanaohusika na udhaifu hawachukuliwi hatua ilhali ripoti inawasilisha ushahidi imara. Ni wazi kwamba rasilimali zilizopo hazitumiki ipasavyo na kwa kufuata vipaumbele. Lakini bado Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii katika ripoti yake ya mwaka 2007/08 anaelezea kuwa wizara imeboresha udhibiti wa ndani wa matumizi.

Serikali ya Tanzania bado inashindwa kutenga asilimia 15 ya bajeti kwa ajili ya afya kama ilivyokubaliwa katika Azimio la Abuja 2001, ambalo limesainiwa na Tanzania. Iwapo mtu atatakiwa kutoa maoni kutokana na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, ni wazi kwamba ongezeko la kiasi cha bajeti kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii halitaboresha huduma inavyotarajiwa na watu.

Kabla ya bajeti ya afya kufikia asilimia 15 ya bajeti kama iliyokubaliwa, kunapaswa kuwa na mfumo unaohakikisha rasilimali zilizopo zinatumika kwa minajili iliyowekwa. Kama hakuna usimamizi unaofaa wa rasilimali chache tulizonazo, je itawekekana kusimamiwa zikiongezeka? Dhima kuu ya timu ya ukaguzi wa matumizi ya umma na jamii kwa ujumlani kuhimiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, ili kuongeza tija na matumizi sahihi ya fedha za walipa kodi. Pia, usimamizi bora wa fedha na uwajibikaji ni sehemu muhimu ya utawala bora na ni vichocheo vya ukuaji wa haraka wa uchumi.